

Aprili 10,2020

Wapendwa Familia za JCPS,

Wiki ya kwanza ya Mafunzo Yasiyo ya Kiasili NTI iko vitabuni na tumefurahishwa sana kushiriki kwa wanafunzi, familia na walimu katika hali ya masomo. Takwimu za awali zinaonyesha zaidi ya 90% ya wanafunzi walikuwa wamewasiliana na mwalimu (walimu) wao katika shule zetu nyingi. Jumanne peke yake, zaidi ya wanafunzi 80,000, walimu na wasimamizi waliingia kwenye Google Classroom na vipindi 23,000. Hilo ni jambo la kushangaza!

Kama vile Dk Marty Pollio alivyokuwa amesema mara kwa mara, tunajua kutakuwa na changamoto kadhaa lakini walimu wa JCPS, wasimamizi na wafanyikazi wako hapa kusaidia wewe na motto wako. Hapa kuna habari mpya:

- Karibu Chromebooks zote 20,000 zilizokuwa zimeitishwa zinapaswa kufikishwa mwishoni mwa siku Jumatatu. Tungali tunawasiliana na familia za ECE kuhakikisha wana kompyuta nyumbani. Pia tunachukua hatua za ziada kutafuta familia ambazo anwani zao haziambatani na rekodi zetu.
- Wanafunzi wote wanapaswa kuwa wamewasiliana na mwalimu(walimu) wao kufikia sasa. Ikiwa motto wako hajatua barua pepe, kuongea, kutuma ujumbe mfupi au kuwa na mawasiliano yoyote tafadhali wasiliana na mwalimu kupitia barua pepe au jaribu kuwacha ujumbe katika shule.
- Familia wazidi kuchukua Choice Boards katika [Viwanda vya Chakula cha Dharura](#) vyetu ambavyo vinafunguliwa Jumatatu, Jumatano na Ijumaa kutoka 10 asubuhi - 1 mchana. Tulichapisha [Choice Boards](#) 53,000 mpya katika Kiingereza na maelfu zingine katika lugha zingine ambazo zilifanywa kupatikana Jumatano. Kuanza Jumatano, Aprili 15 tutakuwa na pakiti 35,000 za daraja maalum za kusoma zitakazopatikana katika viwanda vya chakula. Pakiti hizi zitakuwa tofauti na Choice Boards.
- Wengine wenu wameelezea kufadhaika katika kujaribu kusanikisha PlayStation au Xbox ya mtoto wako kama kompyuta wanayoweza kutumia kupata kazi yao ya shule ya NTI. Hapa kuna tovuti kadhaa ambazo zinaweza kukusaidia kuelewa: <https://www.youtube.com/watch?v=e9HaCNKgAak> au <https://edtechawesomeness.com/2020/03/17/access-google-classroom-with-your-phone-your-xbox-or-your-playstation/>
- Tunajua wengi wenu wanaweza kuwa wakipambana na kubaki nyumbani, kuwa msaidizi wa mwalimu kwa mtoto wako na kushughulika na ktokuwa na uhakika wa nyakati. Hapa kuna [mbinu na mazoezi](#) ambayo yanaweza kusaidia kukabiliana.

Tunatumai wiki hii ya kwanza ya NTI imekuwa njema kwako na kwa motto wako. Walimu wa JCPS, wakuu na wasimamizi watakuwa wepesi iwezekanavyo ili kupata njia mwafaka kwa kila motto kusoma wakati juu usio wa kawaida. Ikiwa una maswali yoyote, jihisi huru kupigia 313-MSAADA katika masaa ya biashara ya siku za wiki. Mnafanya vyema familia za JCPS! Kuwa na wikendi njema na kuwa tayari kwa Wiki ya 2 ya NTI wiki ijayo.